

JAMHURI YA MUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA  
MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME



22/12/2021

TANGAZO LA ZABUNI NA: LGA/067/2021/2022/S/01.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime anapenda kuwatangazia wananchi wote wenye sifa na uwezo kutoka ndani na nje ya Wilaya ya Tarime kwamba anakartibisha maombi kwa zabuni ya uwakala wa kukusanya mapato, katika Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2021/2022 (JANUARI HADI 30 JUNI 2022)

1. ZABUNI YA UWAKALA WA USHURU :

Maelezo ya kazi	Namba ya zabuni
Uwakala wa kukusanya ushuru wa mazao mchanganyiko	LGA/067/2021/2022/S/01/LOT 1
Uwakala wa kukusanya ushuru soko la sirari	LGA/067/2021/2022/S/01/LOT 2

1. SIFA NA MASHARTI YA MWOMBALI:-

- i. Mwombaji awe raia wa Tanzania
- ii. Mwombaji anatakiwa kufanya utafiti kwenye eneo la mapato analotarajia kuomba na kuonyesha kiasi cha mapato atakachokusanya kwa kila mwezi.
- iii. Mwombaji aambataniше kiviuli cha leseni hai ya biashara inayohusika na ukusanyaji wa mapato.
- iv. Mwombaji awe na hai ya usajili wa walipa kodi (TIN) pamoja na hai ya usajili iwapo mwombaji ni kikundi, Ushirika au Kampuni. Iwapo mwombaji ni mtu binafsi awe Raia wa Tanzania na aambataniше barua ya utambulisho wake kutoka kwa Mwenyekiti wa Kiongoji na Kijiji pamoja na kiviuli cha kitambulisho cha mkazi/ Miga kura
- v. Mwombaji awe na Uzoefu wa kazi aliyoomba kwa muda wa mwaka (1) katika kazi ya uwakala wa kukusanya mapato na kuambataniша nakala ya barua ya uteuzi wa kazi hiyo.

- vi. Mwombaji awe na Uthibitisho wa ulipaji kodi (Tax clearance certificate)
- vii. Mwombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri kwa kazi yoyote ile. Pia awe tayari kuheshimu mkataba endapo atafanikiwa. Kubadili jina la mwombaji akiwa anadaiwa ni udanganyifu usioruhusiwa katika kazi hii. Ikibainika hivyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kufutiwa matokeo.
- viii. Mwombaji asiwe mtumishi au Kiongozi katika Halmashauri ya Wilaya ya TARIME.
- ix. Muombaji ataje asilimia atakayolipwa kwa mwezi na Halmashauri katika mapato atakayokusanya.
- x. Uthibitisho wa uwezo wake kifedha (Bank statement) kuanzia Januari 2021 hadi November 2021.
- xi. Muombaji aambatanishe uhalali wa kisheria (Power of attorney) wa mtu atakayehusika na zabuni hii.
- xii. **Uzoefu wa wataalamu au wafanyakazi atakao watumia katika kufanya kazi ya kukusanya ushuru kupitia wasifu wa kila mhusika (CV).**
- xiii. Mwombaji wa zabuni anapaswa kuambatanisha dhamana ya zabuni kwa ahadi [**Bid Security Declaration**]
- xiv. Mwombaji awasilishe mpango kazi unaoonyesha jinsi atakavyotekeleza majukumu yake katika kipindi cha makataba.
- xv. Mwombaji anatakiwa alipe ada ya maombi ya Tshs. 50,000.00 ambayo haitarudishwa. Kwa kutumia Control No. ya Halmashauri.
- xvi. Mwombaji atapatiwa Nyaraka za **Zabuni kutoka Ofisi ya Katibu wa Bodi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime (ofisi ya zamani Bomani) baada ya kulipa ada ya maombi TSHS. 50,000/=**
- xvii. Zabuni hii ipo wazi kwa mtu binafsi, kikundi cha watu kilichosajiliwa Kisheria, Ushirika, Kampuni au Serikali ya Kijiji, ilimradi awe na sifa na uwezo wa kufanya shughuli hizi na awe tayari kuheshimu Mkataba.
- xviii. Mwombaji ambatanishe katika maombi yake tamko la kutojihusisha na vitendo vya Rushwa au ushawishi wa aina yoyote, fomu ya tamko hili imeambatanishwa ukurasa wa mwisho wa kitabu cha zabuni.
- xix. Mwombaji wa Zabuni ataje kazi yake rasmi.

**NB: Mwombaji anaruhusiwa kupata ufafanuzi wa sharti lolote asilolielewa kabla ya kutuma maombi yake.**